EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

# MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI HUDUMA ZA USAIDIZI KATIKA KIPINDI CHA MPITO KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) – KUMBUKUMBU NA 0010006714

TOTAL East Africa Midstream B.V Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika makapuni yanayojishughulisha na Kilimo, Usambazaji au Huduma za Chakula yenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalopita nchi mbili kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania ili kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia eneo la Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka eneo la Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Bomba lina urefu wa kilomita 1,443, ambapo kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litakatiza Mikoa nane (8), ambayo ni; Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Bomba litapita katika Mamlaka za Halmashauri za Wilaya 27 na Vijiji 231

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa EACOP unahitaji mkuza wa ardhi kwa ajili ya bomba na miundo mbinu husika ya juu ya ardhi na kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa Bomba la Mafuta Ghafi. Hivyo Mradi utatwaa ardhi, na kupelekea uhamishaji wa Waguswa wa Mradi pamoja na Kaya zao kutoka kwenye maeneo yao na shughuli zao za kiuchumi.

Ili kupunguza madhara ya uhamishaji, Mradi utatekeleza utaratibu wa usaidizi katika kipindi cha mpito kwa Waguswa na Kaya waliobainishwa kuwa watahamishwa katika makazi yao au maeneo ya shughuli zao za kiuchumi katika Maeneo ya Awali na Mkuza wa Bomba la Mafuta. Usaidizi katika kipindi cha mpito unaojumuisha vifurushi vya chakula, unatolewa kama nyongeza kwenye malipo ya fidia ili kuhakikisha kuwa kaya zinaweza kujikimu mahitaji ya msingi na kutokuyumba kimaisha mara ardhi itakapo chukuliwa hadi watakapo weza kurejea Maisha yao katika hali waliyokuwa nayo kabla ya Mradi.

Mradi unahitaji huduma za kampuni za Kitanzania zenye sifa, uzoefu na zinazoweza kutoa huduma za usaidizi wa kipindi cha mpito kama inavyoelezwa hapa. Mawanda a ya kazi yatajumuisha:

- **Kipengele cha Kwanza Cha Mawanda ya Kazi**: Utafutaji, uhifadhi ghalani, ufungashaji na usambazaji wa vyakula vifuatavyo katika vijiji 231 Bomba la Mafuta linapopita

| | Vijijivinavyoguswa | Mahindi | Maharage | Mchele | Chumvi | Mafuta ya kupikia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Makadirio ya kiwango kwa mwezi | 231 | 161,140 kg | 161,140 kg | 161,140 kg | 8057 kg | 40,285 L |
| Jumla ya makadirio kwa miezi 12 | | 1,933,680 kg | 1,933,680 kg | 1,933,680 kg | 96, 684 kg | 483, 420 L |

- **Kipengele cha Pili cha Mawanda ya Kazi:** Utafutaji, uhifadhi ghalani, ufungashaji na usambazaji wa vyakula vifuatavyo katika vijiji 12 katika Maeneo ya Awali

| | Vijiji vinavyoguswa | Mahindi | Maharage | Mchele | Chumvi | Mafuta ya kupikia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Makadirio ya kiwango kwa mwezi | 12 | 6, 625 kg | 6, 625 kg | 6, 625 kg | 333 kg | 1, 763 L |
| Jumla ya makadirio kwa miezi 12 | | 79, 500 kg | 79, 500 kg | 79, 500 kg | 3,996 kg | 483, 420 L |

**Kipengele cha Tatu cha Mawanda ya Kazi:** Utafutaji, uhifadhi ghalani, ufungashaji na usambazaji wa vyakula vifuatavyo katika vijiji 12 katika Maeneo ya Awali

| | Vijiji vinavyoguswa | Mahindi | Maharage | Mchele | Chumvi | Mafuta ya kupikia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Makadirio ya kiwango kwa mwezi | 12 | 3, 843 kg | 3, 843 kg | 3, 843 kg | 194 kg | 961 L |
| Jumla ya makadirio kwa miezi 12 | | 23, 058 kg | 23, 058 kg | 23, 058 kg | 1,164 kg | 5,766 L |

Pamoja na kutoa kiwango tajwa vya vyakula, makampuni yenye nia yatatakiwa:

- Kupendekeza kwa Mradi mfumo bora wa kutekeleza na kusimamia usambazaji wa vifurushi tajwa vya chakula kwa mpango wa kikapu cha chakula kimoja kimoja kwa kiwango kilichotajwa. Mfumo bora wa kikapu cha chakula NI LAZIMA uruhusu wanufaika kupata vikapu vyao vya vyakula,
- Kuhifadhi, kufungasha na kusambaza vifurushi vya chakula kwa Waguswa wa Mradi pamoja na Kaya zilizoguswa,
- Kuanzisha na kusimamia m/mitandao ya wasambazaji katika maeneo husika kwa kipindi cha mkataba,
- Kufuatilia na kusimamia usafi wa chakula katika maeneo yote ya kufungashia na kuhifadhi, na
- Kufuatilia na kuripoti juu ya mafanikio ya kuwafikishia wanufaika vifurushi vya chakula.
- kuonyesha nia kwa kipengele cha kwanza cha mawanda ya kazi au cha pili au cha tatu au vyote,
- kuonyesha nia ya kutoa huduma katika mkoa mmoja au mikoa kadhaa, lakini Mradi unabaki na haki ya kuto kugawa mawanda katika vipengele vidogo,
- Makampuni yenye nia yanaweza kuingia mkataba wa makubaliano na makampuni mengine ili kuboresha utoaji wao wa huduma, lakini, wabia wote au kila mmoja NI LAZIMA watimize vigezo tajwa hapa chini.

Pamoja na hayo, Mradi unabaki na haki hizi:
- Haki ya kutekeleza mawanda ya kazi kwa hatua, kutoa urahisi wa utaratibu wa kumaliza kazi, Viwango vya muda wa kutoa usaidizi wa kipindi cha mpito uliotajwa unaweza kufupishwa au kuongezwa kutokana na matakwa ya Mradi,

Kiwango cha vyakula kinavyohitajika unaweza kupunguzwa au kuongezwa kutokana na matakwa ya Mradi.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili katika vyombo au taasisi za Kitaaluma za nchini Tanzania (Ikipasa)
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Idhini ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Makampuni yanayotumia wahudumu wa ndani ya nchi NI LAZIMA pia watume nyaraka sawa na hizi kwa watoa huduma,
- Uthibitisho wa taarifa za fedha zilizokaguliwa. Takwa hili ni kwa ajili ya kuweza kufikia matakwa ya Mradi kwamba makampuni yatakayochaguliwa yana rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza mawanda ya kazi inayohitajika,
- Kama makampuni yanayotumia wahudumu wa ndani ya nchi NI LAZIMA pia watume nyaraka sawa na hizi kwa watoa huduma,
- Uthibitisho wa kuwa na mtandao wa watoa huduma katika mikoa iliyotajwa, kuonyesha miundombinu ya kutosha katika kufanikisha usambazaji unaohitajika. Taarifa za mawasiliano ya Mtoa Huduma na eneo husika anapopatikana ziwasilishwe.
- Uthibitisho wa miundombinu ya ghala, ufungashaji na usambazaji katika mikoa iliyotajwa uwasilishwe.Pia taarifa za maeneo na ya hali ya miundo mbinu hii ziwasilishwe,
- Uthibitisho wa uwezo wa kutafuta na kusimamia kiwango cha chakula kinachohitajika ili kufanikisha kazi inayohitajika,
- Uthibitisho wa sera na taratibu za mfumo wa afya na usalama,
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha majibu ya nia kwa ombi hili yanahimizwa.

---

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwakupitia barua pepe:**mihye.allaire@external.total.com** nanakala kwa **talal.mufti@external.total.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia **saa 11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **30th April 2021.**

Mapendekezo ya kifedha yasiwekwe katika Nia hizi.

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**